

Maswali

1. Waisraeli walipigana na nani?
2. Nani alikuwa adui wao na shujaa sana?
3. Alikuwa wa namna gani?
4. Daudi alikuwa nani?
5. Alipigana na nani wakati alikuwa akichunga kondoo?
6. Nani alisema atapigana na Goliathi?
7. Mbona Daudi hakutaka kuva mavazi ya Sauli?
8. Daudi alienda kupigana na Goliathi na nini?
9. Daudi aliuaje Goliathi?
10. Mbona Daudi aliweza kumuua Goliathi?

Majibu

1. Waisraeli walipigana na Wafilisti
2. Shujaa alikuwa Goliathi wa Gathi
3. Goliathi alikuwa jitu
4. Daudi alikuwa kijana mchungaji
5. Daudi alipigana na simba na dubu alipokuwa akichunga kondoo
6. Daudi alisema atapigana na Goliathi
7. Zilikuwa kubwa tena hakuwa amezizoea
8. Daudi alichukuwa fandiri na mawe matano
9. Alipiga Goliathi paji la uso na kukata kichwa
10. Daudi aliamini Mungu

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

24 Daudi na Goliathi

Marejeo

1 Samwel 17

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anaweza kutulinda kutoka kwa adui wenye nguvu


Maneno maalum

1. Wafilisti + vita
2. Jitu + Goliathi + changa moto + siku 40
3. Daudi + Kijana mchungaji + Yesu + Mfalme Sauli + Wafilisti + pigana
4. Daudi + nduguze + Goliathi + changa moto + silaha ya mfalme + kombeo (fandiri) ya mchungaji + mawe matano + Mungu ataoako
5. Goliathi + hakuamini + Daudi + imani + amini Mungu + ua + shujaa wa Israeli

24.1 Wafilisti na Waisraeli walikuwa majirani lakini walikuwa maadui. Wakati hadithi hii iliandikwa kulikuwa na vita kati yao. Pale walipokuwa wakipigania kulikuwa na bonde katikati ya vilima nya Yuda, kila watu walismama ng'ambo yake.

24.2 Wafilisti walikuwa na shujaa aliyeitwa Goliathi wa Gathi. Alikuwa mrefu tena mkubwa (kama futi 9 au mita 3 urefu). Alivaa silaha nyingi sana za vita za kumkinga. Hizi silaha kama kofia na koti zilikuwa za chuma. Alibeba ngao na mkuki kubwa. Kwa siku 40 alijitokeza kando ya kilima na kuwapa Waisraeli waliokuwa ng'ambo ingine changa moto ya kutaka wapigane naye.

24.3 Daudi alikuwa kijana mchungaji wa kondoo ya baba yake. Alikuwa ndiye mdogo kwa watoto wa Yesu wa Bethlehemu. Ndugu zake watatu wakubwa walikuwa askari kwa jeshi la mfalme Sauli wa Israeli. Walikuwa wametoka nyumbani kwenda kupigana na Wafilisti.



Daudi alikuwa akichunga kondoo na mara kwa mara alipigana na simba na dubu waliotaka kuua kondoo. Alikuwa ameani Mungu wa Israeli ndiye aliye muokoa kutoka kwa hao wanyama wakali.

24.4 Daudi alitumwa kwenda kuona ndugu zake na kuwapelekea chakula. Daudi aliwapata kwa uwanja wa vita, wakati Goliathi alitoka akiwapigia kelele na kuwapa changa moto.

Kwa kweli Daudi hakuelewa sababu gani hakukuwa na mtu wa kujibu hiyo changa moto, alisema, kama wangemwamini Mungu, angewaokoa kutoka kwa huyu muovu. Pale pale mfalme alisikia habari ya Daudi na akatuma wamuite. Alitaka kujua vile alipanga kupigana na Goliathi. Alimwambia mfalme Sauli vile Mungu alimsaidia kupigana na dubu na simba. Mungu angemsaidia kupigana na jitu Goliathi. Mfalme Sauli alituma walettee Daudi silaha na wamvae. Zilikuwa nzito sana tena hakuwa amezizoea, akazitoa. Badala yake alichukuwa kombeo (fandiri) na mawe matano aliyo yatoa mtoni.

24.5 Goliathi alipoona huyu kijana anakuja kupiga na naye, hakuamini. Alimpigia Daudi kelele kumtisha. Daudi alimjibu kwamba anaamini Mungu aliye msaidia kupigana na simba na dubu. Kwa kutumia fandiri yake alilinga jiwe kwenye paji la uso wa jitu na kumuua papo hapo. Halafu alikata kichwa cha Goliathi na kumpa mfalme Sauli.

Kwa imani na kumuamini Mungu, Daudi alimuua Goliathi na kuwa shujaa wa Israeli.

